

KIZINGITI NI KIFO

Jackson Kauru

Kwa hísia

1. U me ni nye nye ke sha Mu ngu wa ngu u me ni a da bi sha mi mi
Ki la ni ki ku mbu ka Mu ngu wa ngu ha ti ma ya ma i sha ya ngu


The first system of the musical score is written for piano in G major (three sharps) and 2/4 time. It consists of two staves, treble and bass. The melody is primarily in the treble staff, with the bass staff providing a harmonic accompaniment. The lyrics are written below the staves, aligned with the notes.

ni me ku wa m po le Mu ngu wa ngu ni me ku wa mpo le ni me ku wa m
ki zi ngi ti ni ki fo Mu ngu wa ngu ha po na ku si fu ni me pa ta e

The second system continues the musical score. It features a repeat sign at the end of the first four measures, followed by a final measure. The lyrics continue below the staves.

tu mwe ny ma li te na ta ji ri m ku bwa mwe nye he shi ma zo te
li mu na ka zi ye nye ha dhi na zi fa nya i li ni pa te ra ha

The third system concludes the musical score. It includes a key signature change to A major (four sharps) in the final measure. The lyrics are completed below the staves.



2. Umeninyenyekesha Mungu wangu umeniadabisha mimi, nimekuwa mpole Mungu wangu nimekuwa mnyonge. Kila nikikumbuka Mungu wangu hatima ya maisha yangu, kizingiti ni kifo Mungu hapo nimeshindwa. Kosa lile kubwa walotenda wale Adamu na Eva mle Bustanini, wakala tunda la mti ule uliokatazwa. Wewe Mungu uliwaambia pale mtakapo kula, hakika mtakufa, majivuno na kiburi ndicho kimezaa kifo.

3. Umeninyenyekesha Mungu wangu, umeniadabisha mimi, nimekuwa mpole Mungu wangu nimekushimu. Kila nikikumbuka Mungu wangu hatima ya maisha yangu, kizingiti ni kifo Mungu wangu hapo nimeshindwa. Ninaishi vizuri na wazazi wangu hapa duniani wananitegemea, lakini masikini kama ndoto kifo umefika. Ninaishi vizuri na wazazi wangu hapa duniani wananitegemea, lakini masikini kama ndoto kifo wanibeba.

4. Umeninyenyekesha Mungu wangu umeniadabisha mimi, nimekuwa mpole Mungu wangu nimenyong'onyea. Kila nikikumbuka Mungu wangu hatima ya maisha yangu, kizingiti ni kifo Mungu wangu hapo nakusifu. Nimetunukiwa cheo leo nafurahia sana, sasa nitapendeza, lakini masikini kama ndoto kifo wanikumba. Nimepanga mipango kamili juu ya maisha yangu, sasa nitapendeza, lakini masikini kama ndoto kifo wanifyeka.

5. Umeninyenyekesha Mungu wangu umeniadabisha mimi, nimekuwa mpole Mungu wangu nimenyong'onyea. Kila nikikumbuka Mungu wangu hatima ya maisha yangu, kizingiti ni kifo Mungu wangu ninakuabudu. Nimepata daraja takatifu ninafurahia sana, kuhubiri injili, lakini masikini kama ndoto vyote naviacha. Nimefunga nadhiri za maisha ninafurahia sana, nimekuwa mtawa, lakini masikini kama ndoto kifo chanikuta.

6. Umeninyenyekesha Mungu wangu umeniadabisha mimi, nimekuwa mpole Mungu wangu ninakutukuza. Kila nikikumbuka Mungu wangu hatima ya maisha yangu, kizingiti ni kifo Mungu wangu ninakuabudu. Nina jumba kubwa la fahari lenye kupendeza sana, mwenye heshima zote, Lakini kama ndoto Mungu wangu kifo wanisonga. Kiburi cha binadamu wote Mungu umekikomesha, fumbo uliloliweka, linakupatia utukufu sifa na heshima.